AckySHINE.com

Kufikia mshindo au kufika kileleni kwa mwanamke na mwanamme wakati wa kufanya mapenzi

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Je, mwanamke anaweza kufikia mshindo?

Ndiyo, mwanamke anaweza kufikia mshindo wakati wa kujamiiana. Dalili ya mwanamke kufikia mshindo katika kujamiiana ni ile hali ya pekee ya kujisikia vizuri kimwili. Tofauti na mwanaume, anapofikia mshindo mwanamke hakojoi kitu chochote.

Kwa kawaida mwanaume anakojoa manii wakati wa kujamii ana anapofikia mshindo. Kwa sababu dalili hii ni rahisi kuona baadhi ya watu wanadhani kwamba ni wanaume tu wanaofikia mshindo wakati wa kujamii ana. Lakini hii siyo kweli. Mwanamke pia hufikia mshindo, ingawa siyo rahisi kuuona. The ListPages module does not work recursively.

Je, kwa nini mwanamke akigongwa na uume kwenye uke yaani juu hutoa majimaji kupitia ukeni?

Kugusana kwa kutumia viungo vya uzazi ni njia mojawapo ya kuamsha hisia ya kujamii ana. Kama mwanamke anatoa majimaji baada ya kugusana na uume kwenye uke, i ina maana kwamba ameshikwa na ashiki kubwa. Majimaji hayo yanarahisisha uume kupenya ukeni. Chanzo cha majimaji hayo ni vifuko maalumu vilivyomo ndani ya uke. Njia zipi zinaweza kumletea mwanamke mshindo haraka, na zipi zinamletea mwanaume mshindo haraka?

Jambo la msingi kabisa ni kwamba wote wawili kuwa tayari kwa kujamii ana. Yaani kupendana na kujaliana sana, halafu kuwa tayari kwa tendo hilo kimwili, kimawazo na kiakili. Kutokuwa tayari kwa kufanya mapenzi, kwa mfano kwa sababu ya kuogopa ujauzito, inamzuia mtu yeyote kufikia mshindo. Kama wote wawili mpo tayari, kufikia mshindo au kutofikia kunategemea maandalizi ya awali ya mapenzi. Mnatakiwa kukubaliana jinsi mtakavyofanya mapenzi i i ili kila mmoja wenu aweze kufurahia na kuridhika. Kwa uhakika, kila mwanamke na mwanaume anazo sehemu maalumu ambazo ukigusa basi ni rahisi sana kufikia mshindo. Upeo wa hali ya kujamiiana pia unaweza kufikia kwa kupiga punyeto. Kwa mfano, mwanaume anaweza kugusa uume wake au mwanamke anaweza kusugua taratibu kinembe mpaka anafikia mshindo. Kupiga punyeto ni njia i iliyo salama ya kumaliza hamu ya kutaka kufanya mapenzi na haina athari mbaya kiafya. The ListPages module does not work recursively.

Kwa nini mara nyingi mvulana ni mwepesi sana katika kuanzisha kufanya mapenzi? Na kwa nini mwanaume mara nyingi anafikia mshindo kabla ya mwanamke?

Kwa kawaida i inakubalika kuwa wavulana ndiyo waaanze kuonyesha ishara za kujamiaana na tafiti zimeonyesha kwamba mara nyingi mwanaume anafikia mshindo kabla ya mwanamke. Hii ni ukweli katika sehemu nyingi za dunia. Baadhi ya wavulana wanatumia vibaya uwezo wao wa kufanya mapenzi. Wanafuatafuata wasichana na kuwatongoza i ili wafanye mapenzi katika umri mdogo. Hata hivyo kujamii ana katika umri mdogo kunaweza kusababisha athari nyingi kama vile mimba isiyotarajiwa au kuambukizwa magonjwa ya zinaa. Kwa hiyo, wavulana wanashauriwa kuwa wavumilivu licha ya mivuto hiyo ya kutaka kujamii ana, kwa sababu kwa njia ya kujamii ana ovyo mnahatarisha maisha yenu ya

baadaye. Kuna njia nyingine za kuonyesha mapenzi, kama vile kubusu, kukumbatia, kushikana mikono na hata kupiga punyeto. Kimaumbile, mara nyingi mwanaume anafikia mshindo haraka zaidi kuliko mwanamke. Lakini, mkihakikisha kwamba mwanamke ni tayari kwa kujamii ana na kama mmechukua muda wa kutosha kujiaanda vizuri, mnaweza kufikia mshindo pamoja. Hivyo kuwaletea raha na starehe wote wawili.

Printable AckySHINE Article · https://ackyshine.com/post.php?post=26145